## Kituo cha Kikanda cha kutoa Elimu, Mafunzo na Kutafiti kuhusus Rasilimali za Maji ya Ardhini

### RASIMU YA MKATABA WA UTOAJI HUDUMA

| Huduma Inayotolewa | Mahitaji ya Huduma | Gharama ya huduma | Mda wa Kupokea Majibu |
|---|---|---|---|
| Maswali kuhusu Utafiti wa Maji ya Ardhini | Barua pepe: Tuma swali lako kwa ufupi na njia inayoeleweka kupitia barua pepe.<br>Simu: Piga simu na uwasilishe swali lako kwa njia inayoeleweka.<br>Barua: Wasilisha hitaji lako kwa njia iliyo wazi na fupi kupitia barua iliyoandikwa.<br>Tutembelee ofisini: Panga mkutano wa mashauriano ya ana kwa ana ofisini mwetu. | Hailipishwi | Barua pep au Simu: Siku 1 ya kazi<br>Barua: Ndani ya siku 7 za kazi<br>Ziara ya ofisini: Kwa wakati uliopangwa wa kukutana. |
| Uchunguzi wa Ubora wa Maji katika Maabara | Uchunguzi Kamili wa Kemikali ndani ya maji, Uchambuzi wa Isotopu $^{18}O$ na $^{2}H$, Uchambuzi wa viini kwenye maji, na Uchunguzi wa Radoni ($^{222}Rn$) kwenye maji | o Uchunguzi Kamili wa Kemikali ndani ya maji: Shilingi 4,500 kwa kila sampuli.<br>o Uchambuzi wa Isotopu $^{18}O$ na $^{2}H$: Shilingi 1,500 kwa kila sampuli.<br>o Uchambuzi wa viini kwenye maji: Shilingi 2,000 kwa kila sampuli.<br>o Kupima viwango vya Radoni kwenye maji ($^{222}Rn$): Shilingi 500 kwa saa. | Siku 3 za kazi kwa vipimo vyote |
| Kukodisha Vifaa na Huduma ya Kuchukua vipimo Uwandani | Kifaa cha kupima Radoni: RAD7 (Hupima Kiwango cha Radoni 222), Mita ya Kupima Ueneaji wa Umeme Ardhini ya Syscal (Syscal Resistivity Meter) (Kuchambua mwenendo wa miale ya umeme ardhini ili kutoa | o Kifaa cha kupima Radoni: Shilingi 4,000 kwa siku au Shiling 500 kwa saa.<br>o Mita ya Kupima Ueneaji wa | Kulingana na muda wa kukodisha |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | taarifa kuhusu miundo ya chini ya ardhi), Kifaa cha kupima vigezo vya ubora wa maji kwa ujumla: Multiparameter Kit (Kupima Vigezo vya maji kijumla), Acoustic Doppler Velocimeter (Kupima viwango vya maji ya mito) Vifaa vya GPS vya mkononi (Kupima anwani ya kijiografia ya maeneo) | Umeme Ardhini ya Syscal: Shilingi 30,000 kwa siku.<br>o Kifaa cha kupima vigezo vya ubora wa maji kwa ujumla: Shilingi 4,000 kwa siku au Shilingi 500 kwa saa.<br>o Kifaa cha kupima viwango vya maji mtoni (Acoustic Doppler Velocimeter): Shilingi 4,000 kwa siku au Shilingi 500 kwa saa.<br>o Kifaa cha GPS cha mkononi: Shilingi 1,000 kwa siku. | |
| Uhamasishaji kuhusu Maji ya ardhini | Wasilisha maombi, kwa njia ya maandishi, kuhusu mipango na programu ya uhamasishaji wa umma. | Hailipishwi | **Siku 10** |
| Maswali ya Jumla kuhusu Maji ya ardhini. (Ziara za Ofisini bila miadi.) | Tutembelee ofisini kwa maswali ya jumla kuhusiana na utafiti na usimamizi wa maji ya ardhini | Hailipishwi | **Tutembelee wakati wowote, wanaofika kwanza huhudumiwa wakwanza** |
| Kutoa Mafunzo na Kuwezesha | Wasilisha maombi au mapendekezo, kwa njia ya kuandika, yanayohusiana na programu lengwa ya mafunzo na mipango ya kukuza uwezo | Hailipishwi | **Siku 10** |
| Utoaji wa data ya Utafiti | Wasilisha maombi rasmi yaliyoandikwa kwa Kiingereza au Kiswahili ili kupata data au hati mahususi za utafiti | Hailipishwi | **Ndani ya Siku 7 za Kazi** |
| Usajili wa watoa huduma na bidhaa | Sharti uwe na ustahiki kushiriki katika mchakato wa ununuzi. Toa hati zote zinazohitajika kama ilivyobainishwa. | Hailipishwi | Siku **30** |
| Malipo ya watoa huduma na bidhaa kwa Wakati | Sharti uwe umesambaza bidhaa au kutoa huduma, au kutenda kazi, kulingana na mkataba au agizo la ununuzi/ agizo la huduma. Wasilisha hati kamili za kuagiza malipo ikijumuisha ankara na noti ya uwasilishaji. | Hailipishwi | Siku 30 za kazi baada ya kupokea hati kamili. |

<table>
<tr><td>Maoni na Malalamishi</td><td colspan="2">Wasilisha malalamiko au maoni kwa neno la kinywani, au kwa maandishi kupitia visanduku vya mapendekezo, barua pepe, tovuti, au mawasiliano ya moja kwa moja.</td><td>Hailipishwi</td><td>Majibu ya mapokezi yatatolewa ndani ya siku 3 za kazi. Suluhisho litawasilishwa ndani ya siku 7 za kazi.</td></tr>
<tr><td colspan="5">TUMEJITOLEA KUKUZA UUNGWANA NA UBORA KATIKA UTOAJI HUDUMA<br>Huduma yoyote inayotolewa ambayo haiambatani na viwango vilivyotajwa hapo juu, au afisa yeyote ambaye hazingatii ahadi yetu ya kukuza uungwana na ubora katika utoaji wa huduma, anapaswa kuripotiwa kwa Afisa Mkuu Mtendaji.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Afisa Mkuu Mtendaji<br>Kituo cha Kikanda cha kutoa Elimu, Mafunzo na Kutafiti kuhusus Rasilimali za Maji ya Ardhini.<br>Jengo la NSSF ‘Block A’, Ghorofa ya 16,<br>S.L.P: 41156-00100,<br>Simu: +254208008004<br>Barua pepe: info@rcgw.go.ke</td><td colspan="3">Katibu wa Tume/ Mkurugenzi Mtendaji<br>Tume ya Haki ya Utawala<br>West End Towers, Waiyaki, Nairobi<br>S.L.P 20414-00200 Nairobi<br>Simu: +254-20-2270000/2303000<br>Barua pepe: complain@ombudsman.go.ke</td></tr>
<tr><td colspan="5">HUDUMA BORA NI HAKI YAKO</td></tr>
</table>

Regional Centre on Groundwater Resources Education, Training & Research